

THE NURSES AND MIDWIVES (ESTABLISHMENT OF
THE COUNCIL AND REGISTRATION OF NURSES AND
MIDWIVES) ACT, 1986.

ARRANGEMENT OF SECTIONS

SECTION

1. Short title and commencement.
2. Interpretation.
3. Establishment of the Council.
4. Functions of the Council.
5. Procedure for making inquiries.
6. Appeal against suspension from practice or removal from register.
7. Registrar to the Council.
8. Register of nurses and midwives.
9. Persons entitled to be registered as nurses.
10. Persons entitled to be registered as midwives.
11. Titles of nurses and midwives.
12. Functions and powers of supervisory authority.
13. Form of certificate.
14. Surrender of certificate on removal of name from register.
15. Registration not to confer rights of qualified medical practitioners.
16. Notice of intention to practise and change of address.
17. Keeping of register of cases by midwives.
18. Payment of fees.
19. Offences and penalties.
20. Regulations.
21. Existing nurses and midwives.
22. Repeal of Nursing Sisters Decree and Midwives Decree.

SCHEDULE

1. Composition of the Council.
2. Removal of member from office.
3. Quorum.
4. Voting.

ACT NO. 9 OF 1986.

I ASSENT

Idris Abdul Wakil

IDRIS ABDUL WAKIL
PRESIDENT OF ZANZIBAR
AND
CHAIRMAN OF THE REVOLUTIONARY
COUNCIL.

14th July 1986.

AN ACT TO PROVIDE FOR THE ESTABLISHMENT,
CONSTITUTION AND FUNCTIONS OF THE NURSES'
AND MIDWIVES' COUNCIL, TO PROVIDE FOR THE
REGISTRATION OF NURSES AND MIDWIVES AND
OTHER MATTERS RELATED THERETO AND INCIDENTAL
THEREWITH.

ENACTED BY THE HOUSE OF REPRESENTATIVES
OF ZANZIBAR.

Short title
and
commencement.

1.(1) This Act may be cited as the Nurses
and Midwives (Establishment of the Council and
Registration of Nurses and Midwives) Act, 1986.

(2) The Act shall come into force on such
a date as the Minister may, by notice in the
Gazette, appoint.

Interpretation.

2.(1) In this Act, unless the context
otherwise requires -

"Council" means the Nurses' and Midwives'
Council established under section 3 of
this Act;

"Nurse" means any person who has successfully
completed nursing courses and is capable
and legally recognised to nurse the sick

2/....

and to render services designed to promote health, to prevent diseases and to promote public health for individuals, the family and the nation in every field of nursing;

"Midwife" means any person who has successfully completed the midwifery courses and is capable and legally recognised to render midwifery services in the field of mother child health care, delivery services, pre-natal and post-natal services in the family and public in general;

"Private practice" in relation to a nurse or midwife means otherwise than as an employee of Government;

"Registrar" means the registrar of nurses and midwives appointed under section 9 of this Act;

"Register" means the register of nurses and midwives kept by the Council under section 8 of this Act;

"Registered" means any person registered under section 8 of this Act and "registered nurse" "registered midwife" and "registration" shall be construed accordingly;

"Minister" means the Minister for the time being responsible for health services;

(2) In this Act, Government includes the Revolutionary Government of Zanzibar, the Government of the United Republic and the Commonwealth.

Establishment
of the
Council.

3.(1) There is hereby established a Council to be known as the Nurses' and Midwives' Council.

(2) The composition of the Council and the conduct of its meetings shall be as prescribed in ^{the} Schedule to this Act.

Functions of
the Council.

4.(1) The functions of the Council shall be -

- (a) to keep and maintain a register of nurses and midwives;
- (b) to publish annually in the Gazette as early in the year as possible, and on such other occasions as it may deem fit, the names and particulars of nurses and midwives contained in the register;
- (c) to issue and cancel certificates, to make entry of and amend any particulars thereon and to replace any certificates proved to have been lost or destroyed;
- (d) to advise the Minister on matters concerning nursing and midwifery and nurses and midwives generally;
- (e) to prescribe and regulate syllabuses of instructions and courses of training for nurses and midwives;
- (f) to prescribe and conduct examinations for nurses and midwives, to appoint and fix the remuneration (if any) of examiners, and to decide upon the places where and the time at which such examinations shall be held;
- (g) to prescribe uniforms, badge and other distinctive dresses to be worn by registered nurses and registered midwives;
- (h) to prescribe the duties of the Registrar to the Council;
- (i) to provide by means of standing orders or otherwise for the regulation of its own proceedings;
- (j) to do any other act or perform any other duty necessary to the carrying out of any of the functions herein before in this section mentioned.

(2) Notwithstanding the provisions of subsection (2) of this section, the Council also shall have power to -

- (a) to order the removal from the register of the name of any nurse or midwife :-

- (i) who has died; or
- (ii) who has been absent from Zanzibar for longer than two years:

Provided that any person who has previously been registered in Zanzibar and who has already paid the prescribed registration fee shall be eligible for re-registration on payment of half the fee paid at the initial registration;

- (iii) who has defaulted to the ethics of nurses and midwives;

- (b) to caution, censure, order the suspension from practice, or order the removal from the register of the name of any registered nurse or registered midwife for malpractice, negligence or misconduct, or for disobeying any regulation made under this Act, and to decide upon the termination of any period of suspension, and the restoration to the register of any name so removed:

Provided that where an order is made under this paragraph suspending from practice or removing from the register the name of any registered nurse or registered midwife, such nurse or midwife shall be notified by the Council in writing by registered post of such order and of her right to appeal under section 6 of this Act;

- (c) to appoint any person who is knowledgeable in the field of medicine or health in general to be a supervisory authority for any registered nurse or registered midwife wherever practising:

Provided that the names of such supervisory authorities and other particulars shall annually be published in the Gazette.

Procedure for
making
inquiries.

5.(1) Before acting in accordance with the provisions of this Act relating to the caution, censure suspension from practice or removal from the register of the name of ~~any registered~~ of the ~~name of~~ any registered nurse or registered midwife the Council shall make due inquiry and upon such inquiry shall have power to take or receive evidence, oral or in writing, from any person, either with or without oath or affirmation, and to examine any document, and for the purposes of the inquiry shall be deemed to have the power of a commissioner acting under the Commission of Inquiry to summon witnesses and to call for the production of documents and to enforce the attendance of any person and the production of any document.

(2) At any such inquiry as in subsection (1) aforesaid the Council shall give to any nurse or midwife against whom any malpractice, negligence, misconduct or disobedience is alleged an opportunity to appear before the Council and be heard, and may in its discretion give audience to any other person on behalf of such nurse or midwife.

Appeal
against
suspension
from
practice or
removal from
register.

6.(1) Any person who considers himself aggrieved by any order or decision of the Council suspending him from practice as a nurse or midwife or removing his name from the register may within three calendar months from the notification to him of such decision appeal to a Special Committee consisting of the Chairman and two other persons appointed by the Minister. The Minister may give such terms of reference and such directions as to procedure or otherwise to such Committee as he shall think fit.

(2) The decision of the Committee on any such appeal shall be final. The appeal shall be presented by petition stating the facts and grounds of appeal, and a copy thereof shall be served on the registrar.

(3) On hearing any appeal under the provisions of this section the Committee shall have the like powers in relation to evidence, witnesses and documents as are conferred upon the Council by subsection (1) of section 5 of this Act.

(4) The Committee may dismiss or allow any appeal, or alter or vary the decision of the Council or make any other order which it may think just.

(5) The Committee shall give to any nurse or midwife who appeals an opportunity of appearing before the Committee and being heard, and may in its discretion give audience to any other person on behalf of such nurse or midwife.

Registrar to
the Council.

7.(1) The Council shall appoint a person, whether a member of the Council or not, to be Registrar to the Council, and may in its discretion from time to time replace any person so appointed.

(2) The Registrar, unless he is a person appointed a member thereof, shall not be or act as a member of the Council.

Register of
nurses and
midwives.

8.(1) The Register of nurses and midwives to be kept and maintained by the Council shall contain the names, addresses, qualifications and other particulars of all nurses and midwives entitled to registration. The Registrar shall be charged with the custody of the register, and the making of entries therein.

(2) The form of the register, the parts into which the same is to be divided, the particulars to be entered therein and the conditions for admission to the register or any part thereof shall be such as may be prescribed or imposed by regulations made under this Act.

(3) A copy of the Gazette containing the contents of extracts from the register of nurses or midwives which purport to be published under the authority of the Council shall be prima facie evidence that the person names therein is registered, and the absence of the name of person therefrom shall be prima facie evidence that such person is not registered.

(4) In the case of any person whose name does not appear in such copy of the Gazette as in subsection (3) aforesaid a certificate under the hand of the Registrar shall be conclusive evidence of the fact and date of such person's registration.

Persons
entitled
to be
registered
as nurses.

9. Subject to the provisions of this Act and any conditions for admission to the register or any part thereof imposed by regulations made hereunder, any person shall be entitled to be registered as a nurse :-

- (a) if he has passed the final nursing examination conducted by the Council; or
- (b) if he produces evidence to the satisfaction of the Council that he is certified or registered or that he has been and is still entitled to be certified or registered as a nurse in any country for the time being prescribed in regulations made under this Act; or
- (c) if he produces evidence to the satisfaction of the Council that he is certified or to be certified or registered as a nurse in any country which is not for the time being prescribed in regulations made under this Act, but is a country in which there was at the material time in force a law for the certification or registration of nurses, and the Council is satisfied that the standard of training and examination required for such certification or registration in the said country is not inferior to the standard adopted by the Council; or
- (d) if he produces evidence to the satisfaction of the Council -
 - (i) that he is a person of good character; and
 - (ii) that he has successfully completed a course of training as a nurse of not less than three years' duration in a country in which there was at the material time no law for the certification or registration of nurses, and the Council is satisfied that the standard of such training is not inferior to the standard adopted by the Council:

Provided that if in either of the cases referred to in paragraphs (c) and (d) of this subsection the Council is not so satisfied as therein specified the person seeking registration may be required to pass such examination as the Council shall direct.

Persons
entitled to
be
registered
as
midwives.

10. Subject as in section 8 by the Act provided, any person shall be entitled to be registered as a midwife :-

- (a) if she has passed the final midwifery examination conducted by the Council; or
- (b) if she produces evidence to the satisfaction of the Council that she is certified or registered or that she has been and is still entitled to be certified or registered as a midwife in any country for the time being prescribed in regulations made under this Act; or
- (c) if she produces evidence to the satisfaction of the Council that she is certified or that she has been and is still entitled to be certified or registered as a midwife in any country which is not for the time being prescribed in regulations made under this Act, but is a country in which there was at the material time in force a law for the certification, or registration of midwives, and the Council is satisfied that the standard of training and examination required for such certification or registration in the said country is not inferior to the standard adopted by the Council; or
- (d) if she produces evidence to the satisfaction of the Council -
 - (i) that she is a person of good character; and

- (ii) that she has successfully completed a course of training as a midwife of not less than one year's duration in a country in which there was at the material time no law for the certification or registration of midwives, and the Council is satisfied that the standard of such training is not inferior to the standard adopted by the Council;

Provided that if in either of the cases referred to in paragraphs (c) and (d) of this subsection the Council is not so satisfied as therein specified the person seeking registration may be required to pass such examination as the Council shall direct.

Titles of
nurses and
midwives.

11. Any person registered under the provisions of section 9 or 10 may use :-

- (a) in the case of a nurse the title of Zanzibar Registered Nurse;
- (b) in the case of Midwife, Zanzibar Registered Midwife; and
- (c) in the case of Nurse-Midwife Zanzibar Registered Nurse-Midwife.

with such modification, if any, appropriate to circumstances as may be prescribed by regulations made under this Act.

Functions and
powers of
supervisory
authority.

12. It shall be the duty of every supervisory authority in respect of any registered nurse or registered midwife under his supervision -

- (a) to exercise general supervision in accordance with any instructions issued by the Council;
- (b) to investigate charge of malpractice, negligence, misconduct or disobedience to regulations, and make a full report to the Council of the facts and circumstances of any charge;

- (c) temporarily to suspend from practice any registered nurse or registered midwife if such suspension appears to the supervisory authority necessary:

Provided that ⁱⁿ the event of such suspension the reasons for and circumstances of such action shall be immediately reported in writing to the Council for final decision, and that such suspension shall not, in the first instance, be for a period in excess of eight weeks;

- (d) to report to the Council the name of any registered nurse or registered midwife convicted of any offence and the nature of the offence as soon as possible after the conviction has been reported to him.

Form of
certificate.

13.(1) There shall be issued to every registered nurse or registered midwife a certificate of registration which shall be in the prescribed form.

(2) For the purpose of this section prescribed form means a manner in which such certificate, in the opinion of the Council, or by regulations made under this Act, shall be.

Surrender of
certificate
on removal
of name
from
register,

14. Any person whose name has been ordered to be removed from the register under the provisions of this Act shall within 30 days calendar months of the notification to her of such order or the dismissal of any appeal lawfully made against such order, whichever is the later, surrender to the council any certificate issued to her by the Council, and on her failure to do so without reasonable cause shall commit an offence against this Act and shall be liable on conviction to a fine not exceeding five thousand shillings, and the court before which she is convicted shall order that the certificate be cancelled.

Registration
not to confer
rights of
qualified
medical
practitioners.

15. Registration under this Act shall not confer upon any person any right to be licenced or registered under the laws relating to Medical Practitioners and Dentists, or any laws replacing or amending the same, or to assume any name, title or designation implying that she is by law authorized to practise medicine or surgery, or to grant any medical certificate or any certificate of death or still-born, or to undertake the charge or cases of abnormality or disease in connection with partrition:

Provided that nothing in this section which relates to undertaking the charge of cases of abnormality or disease in connection with partrition shall be construed as prohibiting any person from rendering assistance in an emergency when the services of a duly qualified medical practitioners are not available.

Notice of
intention to
practise and
change of
address.

16.(1) Every registered nurse or registered midwife, before commencing to engage in private practice, shall give notice in writing of her intention to do so to the Registrar.

(2) When any registered nurse or registered midwife who has been engaged in private practice in one place moves to another place for the purpose of their engaging in private practice she shall within one month after such movement give notice in writing thereof to the Registrar.

(3) Every notice under subsection (1) or subsection (2) shall contain such particulars as may be prescribed.

(4) Every registered nurse or registered midwife who fails to comply with the provisions of this section shall be guilty of an offence.

Keeping of
register
of cases by
midwives.

17(1) Every registered midwife shall maintain a register in the prescribed form of all cases which she attends and shall make such register available for inspection by the Council or a supervisory authority as and when required.

(2) Every registered midwife who fails to comply with the provisions of this section shall be guilty of an offence.

Payment of
fees.

18.(1) Every person on receiving certificate of registration as nurse or midwife shall pay such fees as may be prescribed by the Council.

(2) All such fees shall be paid to the Registrar:

Provided that no fee shall be payable on the registration of any nurse or midwife in the public service.

Offences and
penalties.

19.(1) Subject as hereinafter in this subsection and subsection (3) of this section provided, any person who :-

- (a) not being registered as a nurse or midwife; or
- (b) having been suspended from practice as a nurse or midwife by an order of the Council,

habitually or for gain practises as nurse or attends women in childbirth, shall be guilty of an offence;

Provided that no person who is not registered shall be convicted of any offence under this subsection unless :-

- (i) she is a person entitled to be registered as a nurse or midwife under sections 9 and 10 of this Act, as the case may be; or
- (ii) she is a person who has been so registered but whose name has been removed from the register by order of the Council; or

- (iii) she is a person who is or has been possessed professional qualifications as a nurse or midwife which would, but for other provisions contained in either of the said subsections or elsewhere in this Act or in any regulations made hereunder, have entitled her to be so registered.

(2) Any person who :-

- (a) being a person who is not registered as a nurse or midwife -

- (i) takes or uses any title referred to in section 11 of this Act, or the title of registered nurse or registered midwife (either alone or in combination with any other words or letters), or any name, title, addition or description implying that she is registered or that she is registered or that she is recognised by law as a nurse or midwife; or

- (ii) uses any prescribed uniform, badge or otherwise does any act of any kind calculated to lead to the belief that she is registered under this Act or is recognised by law as a nurse or midwife; or

- (b) being a person who registered in any part of the register takes or uses any name, title, addition or description or uses any prescribed uniform, badge or dress or otherwise does any act of any kind calculated to lead to the belief that she is registered in some other part of the register, shall be guilty of an offence.

(3) Any person who :-

- (a) procures or attempts to procure registration or a certificate by making or causing to be made or produced any false or fraudulent statement or document; shall be guilty of an offence.
- (b) deliberately makes or causes to be made any falsification in any matter relating to the register, shall be guilty of an offence.

(4) Any person who is guilty under the provisions of this section, or under the provisions of any other section to this Act for which no penalty has been provided shall on conviction be liable to a fine exceeding five thousand shillings but not exceeding ten thousand shillings or to an imprisonment exceeding three months but not exceeding six months.

Regulations.

20. The Minister in consultation with the Council may make regulations not inconsistent with this Act, for all or any of the following purposes, and aimed at better carrying out of the provisions of this Act:-

- (a) to prescribe the form of the register of nurses and midwives, the part into which the same is to be divided and any particulars to be entered therein additional to those required by the provisions of this Act;
- (b) to regulate the manner in which application for registration as a nurse or midwife shall be made;
- (c) to prescribe countries having qualifications for the certification or registration of nurses or midwives which will be recognised by the Council;
- (d) to impose conditions with regard to the admission to the register or any part thereof of nurses and midwives;
- (e) to regulate the practice of nurses and midwives and to provide for their functions;
- (f) to prescribe the manner in which nurses and midwives may be suspended from practice and the names of nurses or midwives may be removed from the register, and the procedure for termination of suspension and restoration to the register of the names of nurses or midwives removed therefrom;
- (g) to prescribe the form of certificate and any particulars to be contained therein additional to those required by the provisions of this Act;

- (h) to impose conditions with regard to the issue of certificates to nurses and midwives;
- (i) to prescribe modifications to the titles to be used by registered nurses and registered midwives;
- (j) to prescribe the particulars required to be given in any notification or notice given or issued under this Act;
- (k) to prescribe the fees to be charged for any act or thing done under this Act;
- (l) to prescribe any forms to be used under this Act;
- (m) to prescribe any further matter which is to be or may be prescribed under this Act.

Existing
nurses and
midwives.

21.(1) All nurses and midwives in the public services shall, for the purposes of this Act be deemed to be registered nurses and registered midwives respectively.

(2) Such registered nurses and registered midwives shall be listed in the register and be issued with certificate of registration as soon as may be practicable.

Repeal of
Nursing
Sisters
Decree and
Midwives
Decree.

22. The Nursing Sister (Retiring Allowances) Chapter 46 of the Laws of Zanzibar and the Midwives Decree, Cap.71 of the Laws of Zanzibar and all the rules made thereunder are hereby repealed.

SCHEDULE

UNDER SECTION 3(2)

Composition
of the
Council.

1. The Nurses' and Midwives' Council shall consist of :-

- (a) Director of Medical Services as the Chairman;
- (b) Chief Nursing Officer;
- (c) Principal Nursing Officer;
- (d) Senior Nursing Officer as a member;
- (e) Manpower Officer;
- (f) The Principal, Nurses Training Centre as a member;

- (g) Chief Matron Pemba;
- (h) Matron Mental Hospital;
- (i) Staff nurse appointed by the Minister.
- (j) Midwife appointed by the Minister;
- (k) Two doctors appointed by the Minister as members:

Provided that members appointed under clause 1(i) (j) and (k) shall hold office for a period of 3 years and may be eligible for re-appointment for another period of one term and no longer.

- (1) Not more than two other persons whom the Minister may think fit.

Removal of
member
from
office.

2. A member shall cease to be a member of the Council if -

- (a) he dies while in office;
- (b) he is unable to discharge his duties due to physical or mental inability;
- (c) he resigns;
- (d) he is a member by virtue of his post, if he relinquishes that post;
- (e) he absents himself from three consecutive meetings without reasonable cause;
- (f) he is an appointed member, if he is dismissed.

Quorum.

3. Half of the members shall constitute a quorum.


Voting.

4. The voting shall be by a simple majority and the Chairman shall, in addition to his deliberate vote have a casting vote.

5. The Council shall regulate its own procedure and rules of conduct.

6. The Council may exercise its powers, functions and duties notwithstanding any vacancy in the membership of the Council.

Passed in the House of Representatives, Zanzibar, this 13th day of June, 1986.



SALUM MZEE
ACTING CLERK TO THE HOUSE
OF REPRESENTATIVES.

SHERIA YA KUANTISHA BARAZA LA WAKUNGA NA WAUGUZI,
KUELEZA WAJUMBE NA KAZI ZAKE, UANDIKISHAJI WA
WAUGUZI NA WAKUNGA PAMOJA NA MAMBO YANAYO-
HUSIANA NA HAYO.

Imetungwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

Kifungu:

1. Jina na tarehe ya kuanza kutumika.
2. Ufafamuzi.
3. Uanzishwaji wa Baraza.
4. Kazi za Baraza.
5. Utaratibu wa kufanya uchunguzi.
6. Rufaa dhidi ya kusimamishwa kazi au kufutwa toka kwenye orodha.
7. Mrajis wa Baraza.
8. Orodha ya Wauguzi na Wakunga.
9. Mtu anaestahiki kuandikishwa kama Muuguzi.
10. Mtu anaestahiki kuandikishwa kama Mkunga.
11. Majina ya Wauguzi na Wakunga.
12. Kazi na uwezo wa msimamizi mwenye mamlaka.
13. Umbile la Shahada.
14. Kurudisha shahada baada ya kufutwa.
15. Kuandikishwa hakutoi haki ya kutibu.
16. Notisi ya azma ya kufanyakazi na kubadilika anwani.
17. Wakunga kuweka kumbukumbu.
18. Malipo ya ada.
19. Makosa na adhabu.
20. Kamuni.
21. Wauguzi na Wakunga waliopo.
22. Kufutwa kwa sheria ya Wauguzi.

JADWILI YA KWANZA

CHINI YA KIFUNGU CHA 3 (2)

1. Wajumbe wa Baraza.
2. Kuachishwa kazi.
3. Kufanyika mkutano.
4. Kupiga kura.
5. Utendaji kazi wa Baraza.
6. Nguvu za Baraza.

SHERIA NAMBA ...9.49.1986

NAKUBALI

Ibrahim Abdulwahid

IDRIS ABDULWAKIL
RAIS WA ZANZIBAR
NA MWENYEKITI WA
BARAZA LA MAPINDUZI

14th July, 1986

SHERIA YA KUENZISHA BARAZA LA WAKUNGA NA
WAUGUZI, KUELEZA WAJUMBE NA KAZI ZAKE,
UANDIKISHAJI WA WAUGUZI NA WAKUNGA PAMOJA
NA MAMBO YANAYOHUSIANA NA HAYO

IMETUNGWA na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

Jina na
tarehe ya
kuanza
kutumika.

1. (1) Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Wauguzi na Wakunga (Uanzishaji wa Baraza na Uandikishaji wa Wauguzi na Wakunga) ya mwaka 1986.

(2) Sheria hii itaanza kutumika katika tarehe ambayo Waziri ataitangaza kwenye Gazeti Rasmi la Serikali.

Ufafanuzi.

2. Katika Sheria hii, isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo -

"Baraza" maana yake ni Baraza la Wauguzi na Wakunga kama lilivyoainishwa chini ya kifungu cha 3 cha Sheria hii;

"aliyeandikishwa" ni mtu ye yote aliyeandikishwa chini ya kifungu cha 9 cha Sheria hii;

"kazi ya Kibinafsi" kuhusiana na Muuguzi au Mkuunga ni ile kazi anayofanya ambayo ipo nje ya kazi za Serikali;

"Muuguzi" ni mtu aliyehitimu na kufaulu mafunzo ya Uguzi na kukubalika Kisheria kutoa huduma za Uguzi katika kuendeleza afya, kukinga maradhi, kuwahudumia wagonjwa na kuimarisha afya ya wanadamu - peke yake, familia, jamii na hadi taifa zima, katika kila fani ya taaluma hiyo.

"Mkunga" ni mtu aliyehitimu, kufalu na kukubalika kisheria kutoa huduma za ukunga katika utunzaji wa afya ya mama wajawazito, kuzalisha, huduma za wazazi na afya bora ya watoto hadi kukua kwao katika familia na jamii;

"Mrajis" maana yake ni Mrajis wa Wauguzi na Wakunga alieteuliwa chini ya kifungu 7 cha Sheria hii;

"orodha" maana yake ni orodha ya Wauguzi na Wakunga itakayowekwa na Baraza chini ya kifungu cha 8 cha Sheria hii;

"Waziri" maana yake ni Waziri ambaye kwa wakati huu anashughulikia mambo ya Afya.

(2) Katika Sheria hii neno Serikali linajumuisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Serikali ya Muungano na Jumuiya ya Madola.

Uanzishwaji wa Baraza.

3. (1) Baraza linaanzishwa litakalojulikana kama ni Baraza la Wauguzi na Wakunga.

(2) Wajumbe wa Baraza pamoja na mikutano yake itakuwa kama itakavyoainishwa na Jadwali ya kwanza ya Sheria hii.

Kazi za Baraza.

4. (1) Kazi za Baraza zitakuwa -

(a) kuweka na kutunza orodha ya Wauguzi na Wakunga;

(b) kuchapisha Gazetini mapema kila mwanzoni mwa mwaka au wakati mwengine litakapoona inafaa, majina pamoja na habari nyengine za Wauguzi na Wakunga, habari ambazo zimo katika orodha;

- (c) kutoa na kubatili shahada, kuongeza au kurekebisha jambo lolote lililomo ndani ya orodha hiyo na kuifuta shahada yo yote ambayo itakuwa imepotea au kuharibika;
- (d) kumshauri Waziri kuhusiana na masuala ya uuguzi na ukunga pamoja na Wauguzi na Wakunga kwa ujumla;
- (e) kuanzisha na kusimamia muhtasari wa masomo na kazi za mafunzo kwa wauguzi na wakunga;
- (f) kutunga na kusimamia mitihani kwa Wauguzi na Wakunga, kuweka marupurupu (kama inafaa) kwa watahini pamoja na kuamua pahala na wakati wa kufanyia mitihani hiyo;
- (g) kuweka sare, beji na nguo maalum kwa Wauguzi na Wakunga walioandikishwa;
- (h) kueleza kazi zitakazofanywa na Mrajis wa Baraza;
- (i) kueleza kwa njia ya Amri ya Kudumu au njia nyengine taratibu za kuendesha shughuli zake;
- (j) kufanya jambo lolote jengine ambalo ni muhimu kwa utekelezaji wa kazi yoyote kati ya kazi zilizoелеzwa kwenye kifungu hiki.

(2) Bila ya kutegemea maelezo yaliyomo ndani ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, Baraza pia litakuwa na uwezo wa -

- (a) kuamuru kufutwa kutoka kwenye orodha jina la Muuguzi au Munga ye yote -
 - (i) ambae amekufa; au
 - (ii) ambae hakuwepo Zanzibar kwa zaidi ya miaka miwili;

Isipokuwa mtu ye yote ambae mwanzoni aliandikishwa Zanzibar na kulipa ada inayotakiwa anaweza kuandikishwa tena baada ya kulipa musu ya ada aliyoitoa alipoandikishwa mwanzo.

- (iii) ambae amekwenda kinyume na maadili ya Wakunga na Wauguzi;

- (b) Kuhadharisha, kuonya, kusimamisha kazi, au kuamuru kufutwa toka kwenye orodha, jina la Muuguzi au Mkunga ye yote kwa sababu ya mwendo mbaya, dharau au ukosefu wa nidhamu, au kwa kutofuata amri yo yote iliyotolewa chini ya Sheria hii, na kuamua kufuta amri ya kumsimamisha kazi pamoja na kumrudisha kwenye orodha jina lolote ambalo mwanzoni lilifutwa;

Isipokuwa pale amri inapotolewa chini ya aya hii ya kumsimamisha kazi au kulifuta jina lake katika orodha, Muuguzi au Mkunga huyo ataarifiwa kwa maandishi na Baraza pamoja na kujiilishwa haki yake ya kukata rufaa chini ya kifungu cha 6 cha Sheria hii iwapo hakubaliani na uamuzi wa Baraza.

- (c) kumteua mtu ye yote ambae ni mtaalam katika nyanja ya tiba au afya kuwa ni msimamizi wa Muuguzi wa Mkunga ye yote aliyeandikishwa.

Isipokuwa itakuwa ni lazima majina ya wasimamizi hao pamoja na maelezo yao mengine yatolewe Gazetini kila mwaka.

Utaratibu wa kufanya uchunguzi.

5. (1) Kabla ya kuchukua hatua chini ya Sheria hii za kuhadharisha, kuonya, kusimamisha kazi au kufuta jina la Muuguzi au Mkunga ye yote, Baraza litafanya uchunguzi na katika uchunguzi huo, litakuwa na uwezo wa kupokea ushahidi wa mdomo au wa maandishi, na kwa madhumuni ya uchunguzi huo, Baraza litahesabiwa kuwa na uwezo wa kamishna anaefanya kazi chini ya Kamisheni ya Uchunguzi wa kuweza kumwita shahidi au hati zo zote.

(2) Katika uchunguzi wo wote wa namna hiyo iliyoelezwa kwenye kifungu kidogo cha (2), Baraza litawajibika kumpa haki Muuguzi au Mkunga huyo anayedaiwa kuwa na mwendo mbaya, dharau, ukosefu wa nidhamu au kutotii amri za wakubwa wa kazi, ya kujieleza mbele ya Baraza na iwapo litaona vyema, Baraza linaweza kumtaka mtu ye yote kumwakilisha Mkunga au Muuguzi katika utetezi wake.

Rufaa dhidi ya kusimamishwa kazi au kufutwa toka kwenye Orodha.

6. (1) Mtu ye yote ambaye anahisi kakuridhika na amri au uamuzi wowote wa Baraza wa kumsimamisha kazi kama ni Muuguzi au Mkunga au wa kufuta jina lake kutoka kwenye orodha, anaweza, katika kipindi kisichozidi miezi mitatu tokea utolewe uamuzi, kukata rufaani kwa Kamati Maalumu iliyochaguliwa na Waziri na mbayo itakuwa na Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wengine wawili. Waziri anaweza kuipa Kamati hiyo kumbukumbu na miongozo mengine ambayo anaona inafaa katika kuendesha shughuli zake.

(2) Uamuzi wa Kamati katika rufaa yo yote ya aina hiyo utakuwa ni wa mwisho. Rufaa itakatwa kwa kupeleka malalamiko yatakayoelezea sababu za kukata rufaa na nakla ya malalamiko hayo itapelekwa kwa Mraji.

(3) Katika kusikiliza rufaa yo yote chini ya kifungu hiki, Kamati itakuwa na uwezo kama ule wa Baraza kuhusu mambo ya ushahidi, mashahidi na hati kama ulivyoainishwa chini ya kifungu cha 5(1) cha Sheria hii.

(4) Kamati inaweza kuikataa au kuikubali rufaa yo yote, au kubadili uamuzi wa Baraza au kutoa amri nyengine zinazofaa.

(5) Kamati itampa haki ya kusikilizwa Muuguzi au Mkunga anaekata rufaa na kwa kutumia uwezo wake inaweza kumruhusu mtu ye yote kumwakilisha Muuguzi au Mkunga huyo.

Mraji wa Baraza.

7. (1) Baraza litamteua mtu miongoni mwa Wajumbe wa Baraza au kutoka nje kuwa ni Mraji wa Baraza hilo, na kwa kutumia uwezo wake Baraza linaweza kumbadili Mraji huyo na kumteua mwengine.

(2) Mraji hatokuwa na wala hatofanya kazi kama ni mjumbe wa Baraza isipokuwa anapoteuliwa kuwa ni mjumbe wa Baraza.

Orodha ya Wauguzi na Wakunga.

8. Orodha ya Wauguzi na Wakunga ambayo itawekwa na kutunzwa na Baraza, itakuwa na majina, amani, kiwango cha elimu pamoja na mambo mengine muhimu yahasuyo Wauguzi na Wakunga walioandikishwa. Mraji atakuwa ni mwenye kuenzi orodha hiyo na atawajibika kuingiza maandishi yote kila itakapohitajika.

(2) Muundo wa daftari au orodha hiyo, mgawanyo, mambo yatayoingizwa pamoja na masharti ya uingizaji ndani ya daftari hilo au sehemu yake, yatakuwa kama vile yataka-vyoelezwa na kamuni zitakazotunzwa chini ya Sheria hii.

(3) Nakla ya Gazeti yenye habari inayotoka kwenye orodha ya Wauguzi na Wakunga iliyochapishwa kwa amri ya Baraza itakuwa ni ithubati kamili kwamba mtu aliyetajwa kwenye nakla ya Gazeti hilo kuwa ameandikishwa na kutokuwemo jina lake kwenye nakla hiyo itakuwa ni tihibati kuwa mtu huyo hakuandikishwa.

(4) Katika kesi ambayo jina la mtu ye yote halijatoka kwenye nakla ya Gazeti kama kwenye kifungu kidogo cha (3), shahada iliyotolewa na ^Mrajiis kuhusiana na mtu huyo itakuwa ni ushahidi kamili kwamba mtu huyo ameandikishwa.

Mtu anaestahiki kuandikishwa kama Muuguzi.

9. (1) Kulingana na masharti chini ya Sheria hii na masharti mengine yoyote ya kuingizwa kwenye orodha, au kamuni zitakazotungwa chini ya sheria hii, mtu ye yote atastahiki kuorodheshwa kama ni Muuguzi -

(a) iwapo amefaulu mtihani wa mwisho uliosimamiwa na Baraza; au

(b) iwapo atatoa ushahidi utakaokubaliwa na Baraza kwamba yeye ni Muuguzi mwenye cheti au aliyeandikishwa au kwamba alistahiki na bado anastahiki kupata shahada au kuandikishwa kama Muuguzi katika nchi yoyote ambayo imeelezwa katika kamuni zilizotungwa chini ya Sheria hii; au

(c) iwapo atatoa ushahidi utakaotosheleza Baraza kwamba anayoshahada au anastahiki kupata shahada au kuorodheshwa kama ni Muuguzi katika nchi yoyote ambayo kwa sasa haikutajwa katika kamuni zilizotungwa chini ya Sheria hii lakini ni nchi ambayo katika wakati huo kulikuwepo sheria ya kuthibitisha au kuorodhesha Wauguzi, na kwamba Baraza limeridhika kuwa kiwango cha mafunzo na mitihani kwa Wauguzi wa nchi hiyo siyo cha hali ya chini kulingana na kiwango kilichokubaliwa na Baraza; au

(d) iwapo atatoa ushahidi wa kuweza kutosheleza Baraza -

(i) kwamba yeye ni mtu mwenye tabia nzuri; na

(ii) kwamba amefaulu vizuri kozi ya mafunzo ya uuguzi isiyokuwa chini ya miaka mitatu katika nchi ambayo kwa wakati huo hakukuwa na sheria ya kuthibitisha au kuorodhesha Wauguzi lakini Baraza limeridhika kwamba kiwango cha mafunzo hayo siyo cha hali ya chini kulingana na kiwango kilichowekwa na Baraza:

Isipokuwa tu iwapo katika kesi chini ya aya ya (c) na (d) ya kifungu kidogo hiki Baraza halijaridhika na sifa za mtu anayetaka kuandikishwa kama Muuguzi, basi mtu huyo atatakiwa kwanza afaulu mtihani atakaopewa na Baraza.

Mtu anaestahiki kuandikishwa kama Mkunga.

10. Kwa kuzingatia yaliyoelezwa kwenye kifungu cha 8 cha Sheria hii, mtu ye yote atastahiki kuandikishwa kama mkunga iwapo -

(a) amefaulu mtihani wa mwisho wa ukunga uliosimamiwa na Baraza; au

(b) iwapo atatoa ushahidi utakaotosheleza Baraza kwamba anayo shahda au anastahiki kuandikishwa au kwamba alistahiki na bado anastahiki kupata shahada au kuandikishwa kama Mkunga katika nchi ye yote ambayo imeelezwa kwenye kamuni zilizotungwa chini ya Sheria hii; au

(c) iwapo atatoa ushahidi utakaotosheleza Baraza kwamba anayo shahada au anastahiki kupata shahada au kuorodheshwa kama ni Mkunga katika nchi yoyote ambayo kwa wakati huo haikutajwa katika kamuni zilizotungwa chini ya Sheria hii lakini ni nchi ambayo kwa wakati huo kulikuwepo sheria ya kuthibitisha au kuorodhesha Wakunga, na kwamba Baraza limeridhika kuwa kiwango cha mafunzo na mtihani kwaWakunga wa nchi hiyo siyo cha hali ya chini kulingana na kiwango kilicho kubaliwana Baraza; au

(d) iwapo atatoa ushahidi wa kuweza kutosheleza Baraza -

(i) kwamba yeye ni mtu mwenye tabia nzuri; na

(ii) kwamba amefaulu vizuri kozi ya mafunzo ya uuguzi isiyokuwa chini ya miaka mitatu katika nchi ambayo kwa wakati huo hakukuwa na sheria ya kuthibitisha au kuorodhesha Wakunga, lakini Baraza limeridhika kwamba kiwango cha mafunzo hayo siyo ya hali ya chini kulingana na kiwango kilichowekwa na Baraza:

Isipokuwa tu iwapo katika kesi chini ya aya ya (c) na (d) ya kifungu kidogo hiki Baraza halijaridhika na sifa za mtu anayetaka kuandikishwa kama Mkunga, basi mtu huyo atatakiwa kwanza afaulu mtihani atakaopewa na Baraza.

Majina ya Wauguzi na Wakunga.

11. Mtu yeyote aliyeandikishwa chini ya kifungu cha 9 au cha 10 -

(a) iwapo ni Muuguzi atatumia jina la Muuguzi wa Zanzibar Aliyeandikishwa;

(b) iwapo ni Mkunga ataitwa Mkunga wa Zanzibar Aliyeandikishwa;

(c) iwapo ni Muuguzi-Mkunga basi ataitwa Muuguzi-Mkunga wa Zanzibar Aliyeandikishwa.

Majina haya yanaweza kutumika hivyo hivyo au kubadilishwa kidogo kulingana na mazingira kama itakavyoelezwa na kamuni zilizotungwa chini ya Sheria hii.

Kazi na uwezo wa msimamizi mwenye mamlaka.

12. (1) Litakuwa ni jukumu la kila msimamizi mwenye mamlaka juu ya Wauguzi au Wakunga walioandikishwa walio chini ya usimamizi wake -

(a) kusimamia kwa ujumla amri zilizowekwa na Baraza;

(b) kuchunguza madai ya mwenendo mbaya, dharau, ukosefu wa nidhamu au kutotii kamuni na

kupeleka ripoti kamili kwa Baraza;

- (c) kumsimamisha kwa muda Muuguzi au Mkunga
ye yote aliyeandikishwa iwapo itakuwa ni
muhimu kufanya hivyo.

Isipokuwa inapotokea hivyo, sababu za kusimamishwa
huko lazima zipelekwe kwenye Baraza kwa maandishi na bila ya
kuchelewa ili Baraza litowe uamuzi wa mwisho, na iwapo
kusimamishwa huko ni kwa mara ya kwanza, basi kutakuwa si
kwa zaidi ya wiki nane;

- (d) kutoa taarifa kwa Baraza, ya Muuguzi au
Mkunga yo yote ambaye amepatikana na hatia kwa
kosa lolote mara tu apatapo taarifa kuhusu
hatia hiyo.

Umbile la
Shahada.

13. (1) Kila Muuguzi na Mkunga aliyeandikishwa
atapewa shahada ambayo itakuwa na umbile maalum lililokubaliwa.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki umbile maalum
lililokubaliwa litakuwa ni lile umbile la shahada lililope-
ndekezwa na Baraza au kamuni chini ya Sheria hii.

Kurudisha
shahada
baada ya
kufutwa.

14. Mtu yeyote ambae imeamriwa afutwe kutoka kwenye
orodha kwa mujibu wa Sheria hii na baada ya kuarifiwa kuhusu
amri ya kufutwa au baada ya kukataliwa rufaa yake, basi
atalazimika kurudisha shahada hiyo katika kipindi cha siku
thalathini na pindi akishindwa kufanya hivyo atahesabiwa
kuwa ni mkosa na kosa likithibiti atatozwa faini isiyozidi
shillingi elfu tano, na Mahkama iliyomtia hatiani itaamuru
shahada yake ifutwe.

Kuandikishwa
hakutoa haki
ya kutibu.

15. Kuandikishwa chini ya Sheria hii hakutatoa haki
kwa mtu ye yote au kumfanya awe sawa na kuwa ameandikishwa
chini ya Sheria ya Madaktari na Madaktari wa meno au sheria
iliyorekebisha sheria hiyo, au kumfanya Muuguzi au Mkunga
huyo awe na jina, cheo au kazi itakayomfanya aonekane kuwa
ameruhusiwa kisheria kuwa daktari au mpasuaji. Vile vile
kuandikishwa chini ya Sheria hii hakutampa shahada ya
udaktari au kumpa uwezo wa kutangaza kifo au kufariki kwa
mtoto mchanga, au kumpa uwezo Muuguzi/Mkunga huyo wa
kutibu maradhi yasiyo ya kawaida au yale yahusianayo na
uzazi:

Isipokuwa ieleweke kwamba hakuna chochote katika maelezo ya kifungu hiki kitakachomzuia mtu ye yote kutoa msaada katika tatizo lililozuka kwa ghafla na pale ambapo hakuna daktari wa kumsaidia mgonjwa muhusika.

Notisi ya azma ya kufanyakazi na kubadilika anwani.

16. (1) Kabla ya kuanza kujidhughulisha na kazi yake binafsi, kila Muuguzi au Mkunga aliyeandikishwa atalazimika kutoa notisi kwa maandishi kumuarifu Mrajiis kuhusu azma yake ya kufanya hivyo.

(2) Pale ambapo Muuguzi au Mkunga aliyeandikishwa na ambaye anafanyakazi ya kibinafsi katika eneo fulani anapoamua kuhama atawajibika kumuarifu Mrajiis katika kipindi kisichozidi mwezi mmoja toka ahame.

(3) Kila notisi chini ya kifungu kidogo cha (1) na cha (2) itakuwa na mambo kama yatakayotakiwa na Baraza.

(4) Mkunga au Muuguzi ye yote atayekwenda kinyume ma maelezo ya kifungu hiki atakuwa ni mkosa.

Wakunga kuweka kumbukumbu.

17. (1) Kila Mkunga aliyeandikishwa ataweka daftari la kumbukumbu ambalo litakuwa katika umbile mahsusi na ambalo litakusanya kesi zote alizozishughulikia na atalionyesha kwa Baraza au msimamizi mwengine iwapo atatakiwa kufanya hivyo.

(2) Mkunga ye yote atakaeshindwa kutekeleza haya yaliyomo katika kifungu hiki basi atakuwa na makosa.

Malipo ya ada.

18. (1) Mtu yeyote atakaepata shahada ya Ukunga au Uuguzi atalazimika kulipa ada kama atakavyoamriwa.

(2) Malipo yote ya ada yatalipwa kwa Mrajiis.

Isipokuwa hakutatakiwa malipo yo yote ya ada kwa Mkunga au Muuguzi anayefanya kazi Serikalini.

Makosa na adhabu.

19. (1) Kwa mujibu wa yake yatakayoelezwa ndani ya kifungu kidogo hiki na kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, mtu ye yote ambaye -

- (a) hakuandikishwa kama ni Muuguzi au Mkunga; au
- (b) ambaye amesimamishwa kufanyakazi ya uuguzi au ukunga kwa amri ya Baraza, kwa kawaida au kwa malipo, akafanyakazi ya uuguzi au kumshughulikia mzazi, atahesabiwa kuwa na makosa.

Ila ifahamike kwamba hakuna mtu ambaye hakuandikishwa atakaetiwa hatiani chini ya kifungu kidogo hiki isipokuwa -

- (i) awe ni mtu anaestahiki kuandikishwa chini ya kifungu cha 9 au cha 10 cha Sheria hii; au
- (ii) awe ni mtu aliyeandikishwa lakini baadae jina lake likafutwa toka kwenye orodha kwa amri ya Baraza; au
- (iii) awe ni mtu mwenye sifa za kitaalamu ambazo kama si kwa masharti yaliomo kwenye Sheria hii au kamuni zake, zingemwezesha aandikishwe kama ni Muuguzi au Mkunga.

(2) Mtu yoyote ambae -

- (a) hakuandikishwa kama ni Muuguzi au Mkunga -
 - (i) akajipa au akatumia jina lo lote kama ilivyoelezwa kwenye kifungu cha 11 cha Sheria hii, au cheo au jina au wadhifa au maelezo yaoreshayo kwamba yeye ni Muuguzi au Mkunga aliyeandikishwa au kwamba anatambulikana kisheria; au
 - (ii) akatumia sare, alama au kufanya jambo lolote kwa madhumuni ya kuwadanganya watu wamuone kuwa yeye ameandikishwa chini ya Sheria hii au kwamba anatambulikana kisheria kuwa ni Muuguzi au Mkunga aliyeandikishwa; au

- (b) ameandikishwa katika sehemu ye yote ya orodha, akatumia jina lo lote, wadhifa au maelezo, au akatumia sare maalum, alama au akafanya matendo fulani kwa madhumuni ya kudanganya watu wamuone kuwa ameandikishwa katika sehemu nyengine ya orodha,

atakuwa amefanya makosa.

- (3) Mtu ye yote ambaye -

- (a) amepata au anayejaribu kupata kuandikishwa au kupata shahada kwa njia ya udanganyifu au akatoa maelezo au hati za uongo, atakuwa na hatia.

- (4) (b) Kwa makusudi akafanya au akasababisha kufanyika mageuzo ya aina yo yote kwenye daftari la orodha; atakuwa na hatia.

- (5) Mtu ye yote ambaye atashtakiwa chini ya kifungu hiki au chini ya kifungu chochote ambacho hakikueleza adhabu , apatikanapo na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi elfu tano lakini isiyozidi shilingi elfu kumi au kupelekwa Chuo cha Mafunzo kwa muda usiopungua miezi mitatu lakini usiozidi miezi sita.

Kamuni.

20. Kwa kushauriana na Baraza, Waziri anaweza kuweka kamuni ambazo hazitakwenda kinyume na Sheria hii, kamuni ambazo zitakusaidia kuleta ufanisi katika utekelezaji wa Sheria hii na zitakuwa kwa madhumuni yafuatayo -

- (a) kubuni muundo wa orodha wa Wauguzi na Wakunga, mgawanyo wake pamoja na uingizaji wa mambo ambayo hayakuelezwa ndani ya Sheria hii;
- (b) kupanga utaratibu utakaofuatwa katika kuomba kuandikishwa kama ni Muuguzi au Mkuunga;
- (c) kubuni nchi ambazo viwango vyake vya Wauguzi na Wakunga vinatambuliwa na Baraza;
- (d) kuweka masharti kwa uandikishaji wa Wauguzi na Wakunga;

- (e) kusimamia kazi za wakunga na wauguzi pamoja na dhamana zao.
- (f) kupanga utaratibu wa kuweza kumsimamisha au kufuta jina la Muuguzi au Munga ye yote, na uataratibu wa kumfukuza kazini na kurudisha jina lake kwenye orodha;
- (g) kubuni umbile la shahada na maelezo mengine kuongezea yale yaliyoelezwa na Sheria hii;
- (h) kuweka masharti kuhusiana na utoaji wa shahada kwa Wauguzi na Wakunga;
- (i) kubuni marekebisho ya vyeo vitakavyotumiwa na Wauguzi na Wakunga walioandikishwa.
- (j) kubuni maelezo yatayotakiwa kuwemo katika notisi yo yote itakayotolewa au kupokelewa chini ya Sheria hii;
- (k) kubuni malipo ya ada yatakayotolewa kwa kitendo cho chote au jambo lolote chini ya Sheria hii;
- (l) kubuni fomu zo zote zitakazotumika chini ya Sheria hii; na
- (m) kutunga kanuni nyengine kwa madhumuni ya utekelezaji mzuri wa Sheria hii.

Wauguzi na
Wakunga
waliopo.

21. (1) Kwa madhumuni ya Sheria hii, wale Wauguzi na Wakunga wote ambao wapo kabla ya kupitishwa Sheria hii, watahesabiwa kuwa ni Wauguzi na Wakunga walioandikishwa.

(2) Wauguzi na Wakunga hao wataorodheshwa kwenye daftari la orodha na watapewa shahada haraka iwezekanavyo.

Kufutwa kwa
sheria ya
Wauguzi.

22. Sheria ya Wauguzi (Posho la Kustaafu), Mlango wa 46, Sheria za Zanzibar na Sheria ya Wakunga sura ya 71 Sheria za Zanzibar sasa zinafutwa.

JADWILI YA KWANZA

CHINI YA KIFUNGU CHA 3 (2)

Wajumbe wa
Baraza.

1. Baraza la Wauguzi na Wakunga litakuwa na
Wajumbe wafuatao -

- a. Mkurugenzi Huduma za Uguzi.
- b. Chief Nursing Officer.
- c. Principal Nursing Officer.
- d. Senior Nursing Officer.
- e. Afisa wa Mafunzo.
- f. Mwalimu Mkuu wa Chuo.
- g. Muuguzi Mkuu Pemba.
- h. Muuguzi Mkuu Mental Hospital.
- i. Muuguzi } Wakuteuliwa
- j. Mkunga }
- k. Madaktari wawili watakaoteuliwa na Waziri,
isipokuwa wajumbe waliochaguliwa chini ya
kifungu cha 1 (1) (j) na (k) watahika dhamana
zao kwa miaka mitatu na wanaweza kuteuliwa tena
kwa kipindi chengine ambapo baada ya hapo
hawataweza kuteuliwa tena.

1. Watu wasiozidi wawili ambao Waziri atahisi
wanafaa.

Kuachishwa
kazi.

2. (1) Mjumbe atasita kuwa Mjumbe wa Baraza
iwapo -

- (a) atafariki;
- (b) hawezi kufanyakazi zake kwa sababu ya
maradhi ya kimwili au kiakili,
- (c) atajiuzulu;
- (d) kama ni mjumbe wa Baraza kutokana na wadhifa
wake, basi pale atapoacha wadhifa huo;
- (e) hatahudhuria vikao vitatu mfululizo vya
Baraza bila sababu maalum;
- (f) kama ni mjumbe wa kuteuliwa, basi pale
atakapoachishwa.

Kufanyika
mkutano.

3. Ili mkutano wa Baraza ufanyike kutahitajika kuwepo musu au zaidi ya wajumbe wote.

Kupiga
kura.

4. Jambo lolote litapitishwa iwapo waliokubali ni wengi kati ya wale waliopiga kura na Mwenyekiti atakuwa na kura ya uamuzi.


Utendaji
kazi wa
Baraza.

5. Baraza litatunga utaratibu wake wenyewe wa utendaji kazi.

Nguvu za
Baraza.

6. Baraza litakuwa na nguvu na kufanyakazi zake hata kama kuna nafasi moja iwazi.

Imepitishwa na Baraza la Wawakilishi tarehe 13 Juni, 1986.



SALIM MZEE
KAIMU KATIBU WA
BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR.